

## **“Biblia Yasemaje...?”**

“Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Bwana, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.”

Leo nahitimisha mfululizo wa makala ambazo zilianza majuma kumi na moja yaliyopita. Makala ambazo kimsingi zilijikita katika namna ya kuyachukulia maandiko.

Kama una swalii lolote kuhusiana na namna ya kuyachukulia na kuyatumia maandiko, tafadhali usisite kuwasiliana nami au mmoja wa wazee wa Kanisa.

Leo kuna mafundisho lukuki kuhusiana na imani, neema na utii. Tunachopaswa kujuua ni kuwa; Mungu alimpa Yesu madaraka yote mbinguni na duniani, Mathayo 28:18. Na kwa kule kuwa na madaraka yote, Yesu alituachia injili inayotakiwa kusadikiwa na kuitii ili tuupate wokovu. Imani pekee iliyojitenga na matendo haiwezi kuokoa. Mafundisho ya waebrania 11 yanathibitisha jambo hili. Tafadhali soma sura hiyo nawe utaona ya kuwa imani pekee yake (Imani pasipo matendo) haikuwaokoa wahenga hawa. Vipi kama Nuhu angekataa kujenga au Ibrahimu angekataa kuondoka? Vipi kama Henoko angetembea na ulimwengu badala ya kutembea na Mungu? Imani yao iliyochangamana na utiifu iliwaokoa. Kama imani pekee ingewaokoa basi hata mashetani yangeokoka (Yakobo 2:19-20).

Sasa, wengi wanaoamini katika Imani pekee na hata walimu wengi wa uongo wanaojidai kuwa ni sehemu ya kanisa leo wangedai kuwa kufundisha utii ni u-sheria. Na mara kwa mara huwaita majjina kama mafarisayo n.k wale wanaotaka kumtii Kristo. Jamani, kifupi ni kwamba, kuhubiri kwamba tunapaswa “kuyafanya yote katika Jina la Bwana,” maana yake ni kuwa tunatakiwa kutimiliza yale ambayo Yesu anaruhusu, hili lisitufanye sisi kuonekana wa-sheria. Kumtii Yesu ni ushahidi wa unyenyekevu na upendo wetu kwake, Luka 6:46; Yohana 14:15; 15:14. Ni maringo tu ndiyo yawezayo kilitazama neno la Mungu na kusimama kinyume chake. Unyenyekevu husimama pale asimamapo Mungu

Tunachotakiwa kutambua linapokuja suala la Kanisa ni kwamba ni Kristo aliyehubiri katika Mathayo 16:18-19, kwamba kanisa ni lake. Ni Kristo aliyesema “Nitalijenga Kanisa langu.” Ni Kristo ambaye ndiye kichwa cha Kanisa na ni mtangulizi wa yote, Wakolosai 1:18. Ndiye aliye mwanzilishi wa imani, Waebrania 5:9. Na kama kichwa na mwokozi wa Kanisa, mwana pekee wa Mungu.

Ndiye anayeamua mtu afanye nini ili aingie katika mwili wake. Na kama vile alivyomfundisha Nikodemo, katika Yohana 3:3-5, mtu hawezi kuuingia ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili. Kwenye mstari wa tano, “mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu” Mara baada ya kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Bwana Yesu, Yesu alifafanua alichomaanisha kwa kusema “kuzaliwa kwa maji na

roho,” kwa kuwaamuru mitume wake “kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi, na kuwabatiza....” Na si hivyo tu, bali ndiye anayefundisha waliobatizwa waishije, kubadilika na kuabudu. Na kwa kweli, endapo mtu amempokea kuwa Bwana. Basi atamtii.

Hapa Brown Trail tunasadiki katika imani itendayo, imani ile inayotupelekea kumtii Bwana wetu Yesu katika yote.

Hatuna udhuru uwao wote maana hatuoni haya (Warumi 1:16).

Sisi ni kundi linalomcha Mungu ambao “tunaamini na kutii”